# SHULE YA UPILI YA SUNSHINE

**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**MTIHANI WA KABLA YA MWIGO 2017**
**MACHI 2017**
**MUDA: 2 ½**

**JINA: ………………………………………………...NAMBA YAKO:………………………**

**DARASA …………………………………SAHIHI YA MTAHINIWA …………………….**

**Maagizo**

(a) Jibu maswali manne pekee.
(b) Swala la kwanza ni la lazima.
(c) Jibu maswali mengine matatu kutoka sehemu zllizosalia, yaani Riwaya, Hadithi Fupi, Tamthilia na Ushairi.
(d) Jibu swali moja moja kutoka kila sehemu.
(e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

| SEHEMU | UPEO | TUZO |
|---|---|---|
| A: KIDAGAA KIMEMWOZEA | 20 | |
| B: TAMTHILIA | 20 | |
| C: DAMU NYEUSI | 20 | |
| D: FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| E: USHAIRI | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**1. SEHEMU YA A: KIDAGAA KIMEMWOZEA ( ALAMA 20)**

Walemavu katika jamii wametengwa badala ya kupendwa. Fafanua kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (al 20)

**2. SEHEMU YA B: TAMTHILIA ( ALAMA 20)**

1. **"**Ya mwananti kiuvunda nti!"

    a) Weka dondoo hili katika muktadha wake.
    b) Tambua tamathali za usemi katika dondoo. (al 2)
    c) Fafanua ukweli wa "Ya mwananti kiuvunda nti!" kwa kurejelea tamthilia nzaima. (al. 14)

2. Fafanua hali ya matibabu katika mi wa Cheneo (al. 20)

**3. SEHEMU Y A C: HADITHI FUPI - Damu Nyeusi**

**i)** Vijana hukumbana na changamoto nyingi katika maisha Jadili kauli hii kwa kurejelea hadithi hizi. (al. 20)

a) Damu nyeusi
b) Danda la usafi
c) Samaki wan chi za joto
d) Tazama na mauti
e) Shaka ya mambo

**ii)** "Leo ni siku ya siku , siku ya nyani kufa ambapo mtiti yote huteleza.

a) Eleza muktadha ya dondoo hili . (al. 4)
b) Eleza sifa mbili za mrejelewa. (al 2)
c) Fafanua changamoto zinazowakabili waafrika wasomi ughaibuni. (al 14)

## 4. SEHEMU YA C: USHAIRI

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1. Haki ya mtu thawabu Kuidai sitasita
Hata 'nipatishe tabu muhula mimi kukita
Kulitenda la wajibu liwe hai au mata
Nitafanya majaribi na inapobidi matata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

2. Haki ha mtu u'ngwana siseme mimi nateta
Sitaukiri ubwna na jeuri unoleta
Na ikiwa ni kuwana sitajali sitajuta
Sikiri kuoneana na kupakana mafuta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

3. Haki ifukie chini ipige na kubuta
'tumbukize baharini 'tazamia kufwata
Ukaifiche jangwani nitakwenda kuileta
Itundike milimani nitawana kuileta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

4. Haki ijingee ngome izungushe na kata
Na fususi isimame iwe inapitapita
Tainuka nishikame haki yangu kukamata
Sifa kubwa mwanamume kuenda huku wasota
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

5. Uungwana siuuzi kwa njugu au kashata
Ahadi za upuuzi na rai kuitaita
Kwa kila alo maize hawi mithili ya bata
Tope yake makaazi na chakula cha kunata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

**Maswali**

a) Bainisha dhamira ya mshahiri (al. 2)

b) Eleza umuhimu wa mbinu zozote mbili ambazo mwandishi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (al. 4)

c) Andika ubeti wanne kwa lugha tutumbi. (al. 5)

d) Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (al. 3)

e) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (al. 2)

  i) Idadi ya mishororo
  ii) Mpangilio wa vina

f) Fafanua toni ya shairi hili (al. 1)

g) Taja nafsineni katika shairi hili (al. 1)

h) Tambua na ueleze maana ya mshororo ufutao (al. 2)

**FASIHI: SEHEMU YA E**

1. Eleza maana ya Sanaa. (al. 1)
2. Thibitisha kuwa fasihi ni Sanaa. (al. 3)
3. Tofautisha kati ya vitendwa wili na methali. (al. 2)
4. Bainisha kati ya ngano za usuli na visaasili. (al. 2)
5. Taja aina tatu za ngomezi za kisasa. (al. 3)
6. Taja aina tatu za sifa. (al 3)
7. Fafanua sifa za mlumbi. (al 6)